SIMULIZI; SITOISAHAU MBEYA
Imeandikwa na Halfani Sudy
Simu 0674 395733

Ilikuwa mara yangu ya kwanza kufika jijini Mbeya. Jiji nililokuwa nalisikia tu hapo kabla na kuliona katika ramani ya Tanzania. Uhamisho wa kikazi wa baba yangu toka Dodoma kwenda Mbeya ndiyo uliotufanya twende Mbeya familia nzima.

Mimi na baba yangu tulitangulia kwenda Mbeya, wakati mama pamoja na mdogo wangu wa kike, Christina walipanga kuungana nasi baada ya wiki moja.

Kwa majina naitwa James Natai, lakini marafiki zangu wengi wa huko Dodoma walizoea kuniita Jimmy. Mtoto wa kwanza katika familia ya Mzee Natai. Katika familia yetu tulikuwa tumezaliwa wawili tu, mimi na mdogo wangu Christina. Baba yangu alikuwa ni muajiriwa wa shirika la umeme Tanesco katika mkoa wa Dodoma. Huku mama yangu akiwa ni mwalimu wa shule ya Msingi Uhuru.

Kitabia mimi huwa napenda sana kusafiri, na safari ya kuelekea Mbeya niliifurahia sana. Nakumbuka tulipanda basi ya Sai baba. Baba alikaa katika siti ya watu wawili, lakini hatukukaa pamoja. Huku mimi

nikikaa siti ya tatu nyuma toka pale alipokuwa amekaa baba. Siti hiyo ya tatu, kwa bahati mbaya au nzuri ilinikutanisha na mtoto wa kike mrembo sana. Nilikaa kwenye ile siti na kutulia.

Nakumbuka hatukusalimia kabisa na yule msichana, alionesha alikuwa na majivuni sana. Alikuwa amevaa jeans nzuri sana ya bluu na kitop cheupe chenye michirizi meusi chini ya kwapa kuelekea kiunoni, huku masikioni akiwa ameweka earphone zenye rangi ya bluu sawa na ile suruali yake ya jeans, alikuwa makini akisikiliza mziki. Nami nilikaa na kufungua zipu ya pembeni ya begi langu, nikatoa kitabu cha riwaya ya Farida. Nilianza kusoma taratibu.

Safari ya kutoka Dodoma kwenda Mbeya kwa kawaida ni ndefu sana. Takribani saa kumi na mbili. Cha ajabu katika saa zote hizo hatukuongea lolote na yule msichana. Tulikuwa kimya. Yeye akisikiliza muziki, mimi nikisoma riwaya. Tulifika jijini Mbeya saa moja jioni. Jiji lilitukaribisha kwa baridi kali sana. Yule msichana nakumbuka alishuka katika stendi ya mabasi ya Meta, pale katika hospitali kubwa ya wazazi.

Wakati mimi na baba tulishuka stendi kuu, Uhindini. Hatukuwa na pakufikia, kumbuka tulikuwa wageni katika Jiji hilo la kijani. Jiji lililozungukwa na milima mingi sana. Jiji lenye rutuba nzuri kwa kilimo, Jiji

lenye idadi kubwa sana ya watu, Jiji lenye kustahili kuitwa Jiji. Tulipanga vyumba katika nyumba ya kulala wageni palepale Uhindini. Wakati tunaingia katika nyumba ile ya kulala wageni, nilibahatika kusoma bango kubwa la jeusi lenye maandishi meupe makubwa, bango lenye jina la nyumba ile ya kulala wageni. 'SOWETO GUEST HOUSE' Baba alipanga chumba chake, nami alinipangia chumba changu. Tulilala katika nyumba ya kulala wageni siku ile.
*****

Wiki tatu baadae nilikuwa nimeshalizoea Jiji la Mbeya japo kwa uchache. Baba alikuwa ameshaanza kazi katika shirika la umeme Tanesco, Mbeya. Nami nikiwa naendelea na kidato cha tano, katika shule ya Sekondari Sangu. Mama na mdogo wangu Christina au Tina kama tulivyozoea kumuita, walikuwa wameshakuja Mbeya nao.

Ndugu yangu Tina alikuwa anasoma kidato cha pili katika shule ya Sekondari Meta. Sasa hatukuwa tunakaa katika nyumba ya kulala wageni tena. Tulikuwa tumeshapanga nyumba nzuri na ya kisasa, katika mtaa wa Forest. Maendeleo yangu kitaaluma shuleni yalikuwa mazuri sana. Nilikuwa nafanya vizuri sana darasani. Kama ilivyo katika shule ya awali kule Dodoma.

Wiki mbili baadae nilipata rafiki, rafiki wa kiume, rafiki mpole na mwenye busara sana. Rafiki wa kweli. Alikuwa anaitwa Richard Chali. Richard alikuwa rafiki mwema sana kwangu. Tuliyependana na kuelewana sana. Tulikuwa tunashirikiana katika masomo na mambo mengine yote pale shuleni. Ilikuwa utakapomuona Richard Chali basi mimi niko pembeni yake, au utakaponiona mimi basi Richard Chali yuko pembeni yangu. Baadhi ya wanafunzi wengine walikuwa wanatuita sisi mapacha, kwa jinsi tulivyoshibana na kuelewana. Ulikuwa upendo wa dhati ulioanza bila sababu maalum.
Ilitokea tu mimi na Richard Chali kuelewana.
Mwanzoni nilidhani labda ukaribu wa viti vyetu darasani ndio uliosababisha tuelewane na Richard Chali, lakini baadae nikagundua hapana ukaribu wa madawati haikuwa sababu, mbona Victor Anyimike na Mgeni Francis nao nilikuwa nakaa nao karibu sana kimpangilio wa meza lakini hawakutokea kuwa marafiki zangu kama ilivyokuwa kwa Richard Chali.
Ukweli ni kwamba urafiki wangu na Richard Chali ulitokea tu....

Maisha ya jijini Mbeya yalikuwa mazuri kwa ujumla. Pengine kuliko hata yalivyokuwa kule mkoani Dodoma. Kitaaluma shule ya Sekondari Sangu ilikuwa tofauti sana na shule ya Jamhuri nikiyosoma Dodoma. Sangu walikuwa makini sana kuhakikisha wanafunzi

wanafaulu vizuri katika mitihani yao ya shule na Taifa. Kwanza walikuwa na program wakiyoiita 'Crash program' hii ilikuwa kwa vidato vyenye mtihani wa Taifa, vidato kama cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita. Walikuwa wanarudi jioni kusoma baada ya vipindi vya kawaida. Pia walimu walikuwa mahiri sana katika masomo wayafundishayo, na mwisho mkuu wa shule alihakikisha wanafunzi wanakuwa na nidhamu siku zote. Siku zilisonga mbele. Na maisha yaliendelea vizuri katika shule hiyo. Ikapita miezi, ikaja wiki na hatimaye ikaja siku. Siku ya jumatatu. Jumatatu Iliyonifanya nichukue kalamu yangu na kuandika Simulizi hii ya kusikitisha sana. Simulizi ya huzuni. Simulizi inayonifanya nitamke maneno haya huku nikitoa machozi.... Simulizi inayonifanya nilie huku nikisema kamwe SITOISAHAU MBEYA!

Ilikuwa jumatatu tulivu. Sawa na jumatatu zingine zilizotangulia. Jumatatu hiyo jioni tulikuwa na 'debate', kati yetu wanafunzi wa kidato cha tano na wanafunzi wa kidato cha nne. 'Debate' ilikuwa inafanyika katika Ukumbi mkubwa wa shule yetu.

Ilivyotimu saa kumi kamili jioni ukumbi mzima ulikuwa umejaa wanafunzi kushuhudia mashindano hayo ya 'debate'. Ingawa 'debate' iliwahusu wanafunzi wa kidato cha nne na wanafunzi wa kidato cha tano. Lakini hadi wanafunzi wa vidato vingine walikuja

kushuhudia. Kwa upande wetu, wanafunzi wa kidato cha tano imani ya ushindi ilikuwa kwetu, kwangu mimi na kwa rafiki yangu kipenzi, Richard Chali. Sisi tulikuwa mahiri katika kutoa hoja, mahiri katika kupinga hoja, mahiri katika kuuliza na kujibu maswali. La zaidi tulikuwa mahiri sana wa kuongea lugha ya kiingereza.

Ulikuwa mpambano mkali sana wa 'debate'. Ilitupasa tutumie akili zetu za ziada ili kuweza kushinda mpambano ule. Wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa wamejipanga vizuri sana, huku wakishangiliwa na wanafunzi wenzao wote wa O-level. Pamoja na vifijo, nderemo na kelele zao. Mimi niliamini tutashinda tu katika 'debate' ile. Maana nasi tulikuwa tumejipanga vizuri sana, huku tukipewa sapoti kubwa na wanafunzi wa kidato cha sita.

'Debate' ilianza, kijana mmoja wa kidato cha nne aitwaye Mnubi Francis ndiye aliyeanza kuongea katika debate ile. Alikuwa kijana mahiri na mwenye akili sana. Nakumbuka Richard Chali alikuwa wa kwanza kuongea kwa upande wetu. Richard Chali alikuwa katika ubora nzuri sana siku ile, alitoa hoja nzuri sana muda wake ulipofika. Watu wengi walichangia. 'Debate' ilikuwa kama ngoma droo. Ilikuwa inasubiriwa hitimisho tu, labda ndio lingetoa mshindi.

Mimi ndiye nilichaguliwa kwenda kutoa hitimisho kwa upande wa wanafunzi wa kidato cha tano. Nakumbuka mada ilikuwa 'Education is better than money' Sisi tulikuwa tunaikubali hiyo mada, wakati wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa wanaipinga.

Wakati nimesimama pale mbele, baada tu ya salamu macho yangu yaliangalia nyuma ya ukumbi ule, ndipo macho yangu yalipoona kitu cha ajabu sana! Mdomo wangu ulishindwa kuongea. Miguu ilikuwa inatetemeka, nilishindwa kabisa kutamka maneno. Ukumbi mzima ulibaki kimya, wakishangaa nimepatwa na nini, maana niliacha kuongea ghafla. Wanafunzi wa kidato cha tano walibaki midomo wazi. Roho zikiwadunda kwa kasi. Walikuwa wanategemea mimi ndiye ningepeleka ushindi darasani kwangu katika mashindano yale ya 'debate'. Sasa shujaa wao nilikuwa nimepatwa na kigugumizi.

Wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa wanashangilia sana, walikuwa wanatamani nishindwe kuongea vilevile ili ushindi uende upande wao kiurahisi. Mimi niliendelea kuganda vilevile, ilikuwa ni kama kuna mtu kashika rimoti ya runinga, na kubonyaza kitufe kilichoandikwa 'pause'.

Ndipo nilipomwona akitabasamu!

Kule nyuma kulikuwa na msichana. Msichana mrembo sana. Msichana yuleyule tuliyekaa katika siti moja wakati nakuja Mbeya kutokea Dodoma. Msichana ambaye alinichunia katika gari la Sai baba, hakutaka hata kunisalimia, hakutaka hata kuniangalia, alikuwa 'bize' na 'earphone' zake, sijui akisikiliza muziki ama aliegesha tu zile earphone masikioni. Majibu anayo yeye. Msichana ambaye alinionesha kama ana kiburi ama pengine alikuwa na nyodo. Msichana ambaye sikuwahi kumjua hata jina lake. Nitamjua vipi wakati hatukuongea lolote ndani ya basi? Cha ajabu, cha kushangaza, cha kustaajabisha kumbe tulikuwa tunasoma shule moja, sikuwahi kumuona hata siku moja shuleni. Leo ndio siku ya kwanza kumuona pale shuleni, na ni siku ya pili kumuona hapa duniani, na sasa alikuwa ananitabasamulia!

Nami nilitabasamu kidogo, nikajitahidi kuongea, sasa sauti ilitoka!

Nilihitimisha ile mada ingawa sio kwa ufanisi mkubwa kama nilivyokuwa siku zote. Nilivyomaliza kuongea moja kwa moja nilienda kule nyuma, alipokuwa yule msichana, cha ajabu alisimama na kunikimbilia. Alinikumbatia kwa furaha sana. Nilijisikia aibu sana, lakini yeye hakujari hata chembe. Macho ya watu wote ukumbi mzima yalikuwa yanatuangalia sisi. Nilijari, hakujari. Tulivyomaliza kukumbatiana tulikaa kwenye viti. Tuliongea mambo mengi sana, ilikuwa ni kama marafiki tuliopoteana kwa muda mrefu sana. Hakuna

aliyekuwa anajua kwamba tulikuwa ni maadui wa kwenye gari ambao sasa tulikuwa marafiki ukumbini. Marafiki wa kweli. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa urafiki wangu na yule msichana niliyekuwa namuona alikuwa na majivuno sana na kiburi hapo kabla. Msichana niliyekuja kumtambua kuwa alikuwa anaitwa Evelyne, Evelyne Gando.

Kwa kuwa Evelyne alikuwa rafiki yangu, moja kwa moja alikuwa rafiki wa rafiki yangu pia, Richard Chali. Sasa kampani yetu ikaongezeka, ikawa kampani ya watu watatu, ninaweza kusema kampani yetu ilikuwa ndio kampani nzuri zaidi pale shuleni Sangu Sekondari. Tulisaidiana kwa kila kitu. Wanafunzi wengine hawakuupenda urafiki wetu, wapo waliosema tunaringa eti kwa kuwa tulikuwa tunajiona tuna akili sana pale shuleni, wengine walisema tunajivuna kwakuwa ni wazuri na mambo mengine mengi. Lakini maneno ya watu hayakuaathiri kabisa urafiki wetu, maneno ya watu ni maneno tu. Yalipitia sikio la kushoto yakapitiliza hadi sikio la kulia. Yakapeperukia kuleeeeee.

*****

Nakumbuka ilikuwa mwezi wa tatu baada ya kukutana na Evelyne Gando, nakuwa rafiki yangu. Ndipo ndoto na mawazo ya ajabu yakaanza kunitawala kichwani

mwangu. Ndoto na mawazo yaliyokuwa yananiambia kwamba nilikuwa nampenda Evelyne Gando. Naam, ndotoni usiku nilioteshwa hivyo, na mawazo mchana yalinipeleka hukohuko.
Nilijitahidi kupingana na mawazo yangu. Lakini ilikuwa kama nafanya kazi ya kutwanga maji kwenye kinu. Yaani ilikuwa hivi, nikiwa nyumbani sebuleni nikiangalia runinga, watu wakibusiana tu kwenye runinga, mimi mawazo yangu yanaenda kwa Evelyne Gando moja kwa moja. Nikitembea barabarani nikiwaona mwanamke na mwanaume wameshikana mikono tu, mawazo yangu moja kwa moja yalinipeleka kwa Evelyne Gando.
Ndio..nilianza kumpenda Evelyne kimawazo mchana na ndotoni usiku.

Ndoto zangu zote zikabadilika, toka katika vitu nilivyokuwa naviota hapo zamani, sasa zilihamia kwa Evelyne, Evelyne Gando. Shuleni nako nilibadilika. nikaanza kumuonea aibu Evelyne Gando. Yalikuwa mabadiliko yaliyowashangaza sana marafiki zangu, Evelyne Gando na Richard Chali.
Sikuwa naweza kuthubutu kabisa kuangaliana na Evelyne Gando uso kwa uso. Aibu zile wanazokuwa nazo wanawake pindi watongozwapo zikanivamia mimi, tena kwa kasi kubwa sana!

Kutoka mawazoni, kupitia ndotoni, hatimaye ikaja duniani, katika dunia halisi. Ikawa kweli. Nilianza kumpenda kweli Evelyne Gando, na upendo wangu kwake ulizidi kila mshale wa sekunde katika saa ulivyokuwa unasogea. Nilikuwa nampenda sana Evelyne, lakini nilikuwa nampenda kimoyomoyo, hakuna aliyekuwa anajua zaidi ya mimi na moyo wangu. Nikaanza kufikiria namna sahihi ya kuwasilisha hisia zangu za mapenzi kwa Evelyne.
Ilikuwa kazi ngumu kuliko kazi yoyote ile unayoijua wewe hapa duniani. Ngoja nikupe taarifa, hadi naingia kidato cha tano sikuwahi kumtongoza mwanamke yeyote yule hapa duniani. Mimi ni aina ya wale wanaume waitwao domo zege. Nilikuwa mwoga balaa.
Pamoja na uwoga wangu lakini sikuwa na jinsi, ilinipasa kumueleza ukweli Evelyne Gando kuwa nilikuwa nampenda. Hisia zangu zilikuwa zinaniambia hivyo, ilikuwa ni ngumu kukaa na hisia hizo moyoni mwangu, hisia zilizokuwa zinaleta humwehumwe kubwa katika moyo wangu, ili kulitoa humwehumwe hilo, ilikuwa ni lazima nimueleze Evelyne kuwa nilikuwa nampenda. Tatizo sasa lilikuwa nitaanzaje?

Uwoga wangu wa kukaa pamoja na Evelyne, sasa ulikaribisha urafiki wa dhati kati ya Richard na Evelyne. Richard na Evelyne wakawa wanaelewana sana. Ukaribu ambao niliufurahia sana, kwa kuwa nilijua siku za karibuni tu, Richard atamwita Evelyne

shemeji yake. Nakumbuka ilikuwa siku ya alhamisi jioni. Kulikuwa na mechi ya mpira wa miguu pale shuleni kwetu, kati ya shule yetu na shule ya Sekondari Pandahill. Kwa bahati mbaya mimi sikuwa mchezaji wa mpira, ingawa niliupenda sana kuutazama mchezo huo. Nilipanga siku hiyo nd'o iwe siku ya kumueleza ukweli Evelyne Gando. Nimueleze ukweli kwamba nilikuwa nampenda.

Nakumbuka tulikaa pembeni ya uwanja tukiwa watatu, mimi, Richard Chali na Evelyne Gando. Nilikuwa natamani Richard Chali atoke ili nipasue jipu! Nimueleze Evelyne Gando juu ya hisia zangu zilizojificha moyoni. Hisia nzuri toka kwangu kwenda kwa Evelyne Gando. Kila sekunde nilikuwa namuomba Mungu ili Richard Chali atoke tubaki wawili ili nimueleze Evelyne Gando hisia zangu. Bahati Ilikuwa mbaya kwangu, Richard Chali hakutoka hata kidogo, nilisikitika sana kimoyomoyo.

Mpira uliisha, matokeo yalikuwa tumewafunga shule ya Pandahili magoli mawili kwa moja. Tulirejea nyumbani Pamoja na Richard huku tukimwacha Evelyne akirejea katika hosteli ya wasichana alikokuwa anaishi. Iliniuma sana siku ile, maana nilijipanga vizuri sana siku ile kumueleza ukweli Evelyne, lakini nilishindwa.
Usiku wa siku ile sikulala kabisa!

Nikifumba macho tu nilikuwa namuona Evelyne Gando akiwa amesimama mbele yangu. Nikifumbua macho na kuangalia ukuta, picha ya kuvutia ya Evelyne Gando ilikuwa inajichora pale ukutani. Ukweli mapenzi yangu kwa Evelyne yalinitesa sana. Nilimpenda Evelyne pasi na kifano.

Siku ile sikulala lakini asubuhi niliamka. Nilijiandaa na kwenda shule. Nilikuwa na furaha sana kwenda shule, kwakuwa nilikuwa naenda kukutana na Evelyne Gando, maana kumuona tu Evelyne nilikuwa naridhika, mwanamke aliyeziteka hisia zangu haraka sana!

Muda wa kuingia darasani ulipofika, tuliingia darasani nikiwa na Richard Chali. Baada ya kukaa tu kwenye dawati moyo wangu ulikuwa unadunda vibaya sana. Moyo ulikumbuka kitu, haukuwa umemuona mwanamke unayempenda. Na ilikuwa hivyo, hadi mwalimu wa historia anaingia Evelyne hakuwepo darasani. Mwalimu alikuwa anafundisha lakini sikumuelewa hata kidogo. Mwalimu alivyotoka darasani, na mimi nilikuwa nyuma yake, ndio nilitoka nje. Nilianza kurandaranda katika viunga vya shule kumtafuta Evelyne, Evelyne Gando mwanamke aliyetokea kuziteka hisia zangu. Na kuzipeleka atakavyo.

Nilitafuta katika madarasa mengine, stoo, maofisini kwa walimu mpaka chooni lakini Evelyne Gando sikumuona! Mwishowe nikaamua kwenda kumwangalia Evelyne katika hosteli ya wasichana. Nilihisi labda Evelyne Gando alikuwa anaumwa. Hivyo niliamua kwenda kutafuta hukohuko hosteli kwao! Ngoja nikwambie kitu ...Nilikuwa naenda mahali ambako wanaume hatukuruhusiwa hata kukaribia. Hosteli za kike ilikuwa ni MARUFUKU kwa sisi wanaume kutia pua zetu.

Mimi sijui niliutoa wapi ujasiri, nilipania siyo tu kusogelea eneo hatari la hosteli bali kuingia hadi ndani. Nilikuwa kama chizi, yaani nilikuwa nafanya kitendo hatari zaidi kufanywa pale shuleni. Kukutwa katika bweni la wasichana adhabu yake ilikuwa ni kufukuzwa shule!

Ilikuwa hakuna mjadala.

Ndio Mkuu wa shule hakuwa na masihara kabisa na kosa hilo. kwa maana hiyo kila hatua niliyokuwa napiga kuelekea katika hosteli ya wasichana, ilimaanisha napiga hatua ili nifukuzwe shule. Kila nilivyokuwa nasogelea hosteli ile ya wasichana nd'o nilikuwa nasogelea kufukuzwa shule!

Ilikuwa ni hatari sana lakini sikuhofia hata kidogo.

Nilifika katika nyumba kubwa yenye vyumba vingi ikiyoitwa hosteli pale shuleni. Ilikuwa nyumba kubwa yenye vyumba vingi sana, nilishindwa kuelewa kipi ni chumba sahihi cha Evelyne Gando. Nilienda katika

mlango wa chumba cha kwanza, nilikuta kufuli kubwa aina ya solex inaning'inia pale mlangoni, ishara tosha kwamba hakukuwa na mtu ndani ya chumba. Atakuwa vipi mtu ndani ya chumba ilhali mlango ulikuwa umefungwa kwa nje. Niliangalia milango ya vyumba saba vyote havikuwa na mtu. Niliamini hamna watu kwa kuona ishara ileile, ya kufuli mlangoni. Sasa nilikuwa naelekea katika chumba cha nane, nilikuta mlango ukiwa hauna kufuli!
Ishara kwamba kulikuwa na mtu ndani, au labda iwe amesahau kuufunga. Nilisukuma mlango ule taratibu lakini kwa nguvu kidogo.
Nilichokutana nacho, nilistuka sana!
Nilikuwa natazamana na watu wawili ambao sikuwa natamani kuonana nao kabisa wakati ule. Naam, nilikuwa natazamana na Matron wa hosteli ya wasichana pamoja na mkuu wa shule!

Niliganda pale katika mlango wa hosteli kama sanamu la Michelin. Ghafla nikatoka kwenye usanamu nikarudi katika ubinadamu. Nilipata mstuko mkubwa sana! Mapigo yangu ya moyo yalipiga kwa nguvu mara mbili, Pa..Pa! Pigo la tatu la moyo wangu hata mwenyewe sikulisikia. Nilikuwa nimezimia!

Sielewi nini kilitokea baada ya hapo, lakini nakiri kuwa siku ile baada ya kuamka ndio niligundua kwamba nilikuwa nampenda sana Evelyne Gando, lakini pia

niligundua kuwa nilikuwa namuogopa sana mkuu wa shule ya Sekondari Sangu, Mwalimu Bukuku.

Niliamka toka huko nilikokuwa nimezimia saa nne asubuhi. Nilianguka katika mlango wa hosteli ya wasichana Sangu, niliamka katika hospitali ya mkoa wa Mbeya. Nani alinipeleka? Sikuwa najua. Saa nne asubuhi! Inamaana niliondoka duniani takribani saa nne. Naam, nilizimia saa moja asubuhi, nilizinduka saa nne asubuhi. Nilifumbua macho taratibu nikiwa nimelala kitandani, kwa mbali nilimuona mtu aliyekuwa kasimama pembeni ya kitanda changu nilichokuwa nimelala pale kitandani, nilimtambua vizuri sana mtu huyo, alikuwa anaitwa Evelyne, Evelyne Gando. Baada ya kumuona msichana ninayempenda zaidi hapa duniani. Nilifumbua macho kwa haraka zaidi, kasi tofauti na niliyoanza nayo katika kufungua macho yangu, nia ni kumuona Evelyne Gando.
Nilimuona!

Nilikutana na Evelyne akiwa analia, nilimuangalia kwa umakini, kuanzia chini, nilipofika katika mkono wake wa kulia macho yangu yaliganda, Evelyne Gando alikuwa na bahasha ya kaki katika mkono huo. Baada ya kuiona bahasha ile niligundua kwanini Evelyne alikuwa analia. Lakini sikujari kabisa. Niliushika mkono wake wa kushoto na kuuvuta taratibu ili

nimketishe kitandani, nilifanikiwa, Evelyne alikaa. Baada ya Evelyne Gando kukaa kitandani, huku mimi nikiwa nimelala. Sasa nilitafuta neno sahihi la kutamka kwa wakati ule, ndani ya dakika sita sikulipata neno lolote la maana! Nilichoweza kufanya ni kumwangalia tu Evelyne Gando, bado alikuwa anaendelea kulia. Bila kutegemea, nami nilianza kulia. Sikuwa najua Evelyne Gando alikuwa analia nini, wala sikuwa najua mimi mwenyewe nilikuwa nalia nini, labda nililia kwakuwa Evelyne Gando alikuwa analia!

Huku akiwa analia Evelyne Gando alinipa ile barua aliyokuwa kaishika kwa mkono wake wa kuume, nami bila ajizi nikaipokea, nikanyanyuka kidogo na kuiweka ile bahasha chini ya mto mweupe niliokuwa nimelalia, sikuwa nimeifungua bahasha ile lakini nilikuwa najua kila kitu kilichomo ndani ya bahasha ile. Nilijua Mwalimu mkuu hangeweza kunisamehe kwa kosa la kwenda bila ruhusa katika hosteli ya wasichana, bila shaka yoyote nilijua kuwa ndani ya bahasha ile kuna taarifa ya kufukuzwa shule!
Mwalimu mkuu Bukuku.

Ni nani asiyemjua mwalimu huyo mlokole katika Jiji la Mbeya. Mwalimu ambaye alishawahi kumfukuza shule mwanae wa kumzaa mwenyewe, na siku ya pili asubuhi walipokuwa nyumbani kwao alimuuliza mwanae kwanini haendi shule? ilhali ni yeye ndiye aliyemfukuza

shule jana yake. Ndipo mwanae alimpa barua ya kufukuzwa shule. Mwalimu Bukuku aliisoma barua aliyoiandika mwenyewe kisha akatingisha kichwa, ishara kuwa aliielewa, wakati barua hiyo aliiandika mwenyewe. Mwalimu wa namna hiyo unategemea anisamehe mimi eti kisa nilizimia baada ya kutenda kosa la kuingia katika hosteli ya wasichana?

Baadae niliitoa ile barua chini ya mto na kuifungua! Na kweli baada ya kuifungua barua ile nilikutana na taarifa hiyohiyo niliyokuwa nahisi. Nilikuwa nimefukuzwa shule! Mkuu wa shule, mwalimu Bukuku hakuwa na huruma kabisa, hakujari kuzimia kwangu.
Nikiwa nimeshangaa na barua yangu mkononi, Evelyne Gando alinisimulia jinsi ilivyokuwa sababu ya yeye kutokuja shule, na kilichotokea baada ya mimi kuzimia.
Taarifa aliyonipa Evelyne Gando ilinisikitisha sana. Kumbe naye alikuwepo katika chumba kile cha hosteli nilichoingia kwa pupa bila kujua kuwa ndani yake kulikuwa na watu hatari sana kwa maendeleo yangu ya shule. Labda kutokana na mstuko na fadhaha wa kukutana na mkuu wa shule pamoja na Matron ndomana mimi sikumuona Evelyne Gando mle ndani ya chumba cha hosteli. Evelyne Gando alinieleza kwamba hakuja shule siku ile kwakuwa alikuwa na tatizo. Alikuwa ameibiwa kiasi kikubwa sana cha pesa. Hivyo Matron aliamua kumwita Mkuu wa shule ili

waje kusaidiana katika ushauri namna ya kuwezesha pesa yake irudi. Wakati wanajadiliana nini cha kufanya nd'o ghafla mlango ulisukumwa na mimi, nami kutosema chochote zaidi ya kuzimia baada ya kukutana na sura ya Mkuu wa shule akiwa pamoja na Matroni. Cha ajabu Mkuu wa shule hakustuka wala kujari kabisa juu ya kuzimia kwangu. Wakati Matroni anatafuta jinsi ya kunisaidia, Mkuu wa shule alienda ofisini kwake, Evelyne na Matron walihisi labda anaenda kutafuta usafiri ili waweze kunipeleka hospitali, lakini haikuwa hivyo aliporejea Mkuu wa shule alirudi na barua mkononi, na kuitupa katika kifua changu nikiwa nimezimia.
Ndio, ilikuwa barua ya kufukuzwa shule na hivyo ndivyo nilivyokabidhiwa!

Matroni kwa kushirikiana na Evelyne Gando walijitahidi kunipa huduma ya kwanza, kisha wao ndio walionipeleka hospitali. Ilikuwa hadithi mbaya sana kwangu. Hadithi yenye wahusika wanne, wahusika wawili kati yao wakiwa na roho nzuri, wahusika hao ni Matron na Evelyne Gando. Huku wahusika wawili wakiwa na roho mbaya sana, wahusika hao ni Mkuu wa shule na rafiki yangu kipenzi Richard Chali.
Sina haja ya kuelezea roho mbaya ya Mkuu wa shule nadhani wote mnaijua, kumpa barua ya kufukuzwa shule mtu aliyezimia ni roho mbaya sana. Barua hiyo ingeweza kugeuka kuwa barua ya kifo!

Hebu fikiria mtu unaamka toka katika kuzimia na kukutana na taarifa mbaya, taarifa ya kufukuzwa shule si unaweza kufa kabisa!
Mtu wa pili mwenye roho mbaya ni Richard Chali. Kwa maelezo aliyonipa Evelyne Gando Richard Chali alikuwa anajua kila kitu juu ya kuzimia kwangu, lakini hakujari kabisa, tena alitabasamu baada ya kupewa taarifa ya kuwa mimi nimezimia, baada ya kukutwa katika hosteli ya wasichana. Niliamini maneno ya wahenga walisema kuna mstari mwembamba sana kati ya uadui na urafiki.

Mida ya jioni niliruhusiwa kurudi nyumbani. Nilirejea peke yangu nyumbani. Sikuwa na msaidizi, sikuwa na rafiki, sikuwa na ndugu. Wakati Evelyne Gando alikuwa amesharejea shuleni kuendelea na ratiba zingine, maana aliruhusiwa kunipeleka tu hospitali kwa maana hakukuwa na mtu wakufanya hivyo, rafiki yangu, Richard Chali sikumuona kabisa!

Kumbuka nyumbani hawakuwa na taarifa juu ya kuzimia kwangu. Hilo halikunishangaza sana, kilichonishangaza ni aliyekuwa rafiki yangu kipenzi Richard Chali kutothubutu kabisa kuja kuniangalia.
Nilifika nyumbani saa moja jioni, sikupata ugumu wowote kumueleza baba yangu kuwa nilikuwa nimefukuzwa shule. Baba alikuwa ananipenda sana mimi na familia yake kwa ujumla, alikuwa anampenda

sana mama yangu, pia ananipenda mimi na mdogo wangu Christina. Taarifa ya kufukuzwa kwangu shule kwa kosa la kwenda kumwangalia rafiki yangu katika hosteli za wasichana aliipokea kwa upole huku akiniahidi atanitafutia shule nyingine. Suala la kuhamishwa shule baada ya kukutwa katika hosteli ya wasichana labda ingekuwa ya furaha kwa mtu mwengine, maana lilikuwa kosa lenye chembechembe za aibu, lakini kwangu ilikuwa taarifa mbaya sana! Kuhama shule kwangu ilikuwa na maana ya kutenganishwa na msichana niliyempenda sana hapa duniani, Evelyne Gando. Sikuwa natamani kabisa kuwa mbali na Evelyne Gando, lakini sikuwa na jinsi barua ya ya kufukuzwa shule toka kwa mwalimu Bukuku ilinitaka niwe mbali nae msichana huyo niliyempenda zaidi.

*****

Baada ya wiki mbili nilianza maisha mapya, katika shule mpya kwangu, Shule ya Sekondari Meta. Shule ambayo alikuwa anasoma mdogo wangu Christina. Ukweli ni kwamba sikuwa na furaha kabisa katika shule hii mpya. Wakati wote nilikuwa naiwazia shule ya Sekondari Sangu. Namuwaza Evelyne Gando, sasa hali yangu kimwili ilikuwa mbaya zaidi, nilianza kukonda na kupungua uzito kwa kasi kila siku. Sasa nitaacha vipi kukonda wakati nilikuwa sijamuona

Evelyne Gando wiki ya pili sasa. Nilikuwa nakonda kila mshale wa sekunde wa saa ulivyokuwa unasogea kuelekea upande wa kulia. Siku moja wakati tunakula, baba na mama waliniuliza kwanini nilikuwa napungua sana, lakini sikuwa na jibu la maana la kuwapa. Nitawaambiaje wazazi kwamba nilikuwa nakondeshwa na mapenzi? Nilijiumauma tu, na kusingizia nakondeshwa na masomo. Wote waliniangalia kwa jicho la huruma sana, huku wakinipa pole ya masomo.

Wahenga walisema, mtu atakunyima vyote lakini si rahisi kukunyima maneno. Victor Anyimike ndiye aliyekuja kunithibitishia ukweli wa msemo huo wa wahenga. Victor alininyima vyote wakati tunasoma pamoja pale shuleni Sangu, lakini tulivyokutana pale Mwanjelwa hakuninyima neno. Alinambia habari iliyopasuapasua moyo wangu vibaya sana, eti kwamba kwasasa Evelyne Gando na Richard Chali walikuwa na uhusiano wa kimapenzi huko shuleni Sangu. Ilikuwa ni taarifa mbaya sana kwangu, taarifa iliyosafiri katika mishipa ya damu ya mwili wangu na kwenda kutua katika moyo wangu. Na kuanza kuupasuapasua moyo wangu na kuumiza vibaya sana. Hisia za WIVU zikanitawala moyoni mwangu. Nilipatwa na wivu wa ajabu sana wakati mimi sikuwahi kumueleza hata siku moja Evelyne Gando kuwa nilikuwa nampenda. Chozi la uchungu lilinidondoka hadharani na kupotelea

katika ardhi yenye vumbi ya Mwanjelwa. Sikumbuki hata kama tuliagana na Victor Anyimike.

Nilirudi nyumbani na kujifungia chumbani kwangu na kuanza kulia. Sasa uadui wangu dhidi ya Richard Chali ukakomaa, niwe mkweli tu nilimchukia sana Richard Chali kuliko hata shetani!

"Evelyne Gando hivi ni kweli unanisaliti, Richard Chali hivi ni kweli unanisaliti!" Hayo ndiyo maneno pekee niliyothubutu kusema huku nikiwa natokwa na machozi kitandani.

Nakumbuka nililia sana siku ile. Nilijiona kuwa nimempoteza Evelyne Gando kirahisi sana. Nikiwa nimejilaza pale kitandani nakumbuka mdogo wangu wa kike, Christina aliingia ndani kwangu bila hodi, sijui alifata nini, lakini alichokifata hakukifanya. Alipigwa na butwaa alipogundua kwamba nilikuwa nalia. Kwa mwendo wa taratibu alinifata pale kitandani, alinishika mkono na kwa sauti ya huruma mdogo wangu aliniuliza ni kitu gani kilikuwa kinaniliza lakini nilishindwa kumwambia. Utamwambia vipi ndugu yako wa kike eti unalia kwakuwa umesalitiwa, tena umesalitiwa na mwanamke, mwanamke ambaye hujawahi kumwambia kuwa unampenda.

AIBU ilioje hii.

Niliamua kumdanganya ndugu yangu kuwa nilikuwa naumwa kichwa. Christina aliondoka huku akiwa kichwa chini. Aliamini kweli nilikuwa naumwa, na ugonjwa wangu ulimtia simanzi sana Christina. Nilikuwa mtu mcheshi sana, niliyependa kufurahi muda wote na familia yangu. Lakini leo hii Evelyne Gando na Richard Chali walikuwa wameondoka na furaha yangu. Nililia sana siku ile mwishowe nilinyamaza, niliona kulia hakunisaidii kitu. Nilikaa kitandani na kutafakari kipi cha kufanya. Mawazo mengi yalipita katika kichwa changu. Yalitathminiwa na wazo moja lilikubaliwa kati ya mengi yaliyopita katika kichwa changu. Nikaamua kulifanyia kazi. Niliamua lazima nikutane na Evelyne Gando mahala popote pale ili nimueleze hisia zangu. Nimueleze kuwa nampenda sana. Nataka awe mpenzi wangu. Kisha aje kuwa mke wangu. Mke wangu wa ndoa.

Niliamua siku ya jumapili nikakae pale nje ya geti la shule ya Sekondari Sangu. Ili nisubiri muda wa wanafunzi wa hosteli kwenda kanisani ukifika. Nimfate Evelyne Gando na kumueleza kiasi gani alikuwa ananitesa, kiasi gani alikuwa anautesa moyo wangu, kiasi gani nilikuwa nampenda. Nampenda sana.

Wahenga walisema siku hazigandi.

Pamoja na kuona kwamba siku zinasuasua na kuchelewa sana lakini siku ya jumapili ilifika. Siku ya kwenda kupasua jipu, kwa kueleza hisia za kweli zilizokuwa ndani ya moyo wangu. Nakumbuka jumapili hiyo nilivaa suruali yangu nyeusi ya kitambaa na shati jeupe lenye madoa madoa meusi. Huku chini nikivaa viatu vyeusi vilivyochongoka, maarufu kama mkuki moyoni. Ukweli kwamba nilikuwa nimependeza sana siku hiyo kuliko siku zote.

Tangu saa kumi na moja alfajiri nilikuwa nimekaa nje ya geti la shule ya Sekondari Sangu kumsubiri Evelyne Gando. Mwanamke nikiyemhusudu sana. Saa mbili kamili asubuhi geti lilifunguliwa, na hatimaye nilimuona Evelyne Gando nae akitoka kwa mwendo wa madaha. Evelyne Gando alikuwa amependeza sana siku hiyo.
Alikuwa amevaa suti nzuri za kike za rangi nyeusi, na viatu vyeusi vyenye kisigino kirefu ambavyo vilileta ladha tamu kila Evelyne alivyokuwa akiikanyaga ardhi. Kwa bahati nzuri Evelyne Gando alitoka nje akiwa peke yake, hiyo ilikuwa ni habari njema sana kwangu. Kwa mwendo wa taratibu aliongoza katika barabara ambayo ilikuwa inaelekea njiapanda ya Mafiat, nami nilimfata kwa nyuma huku nia yangu nimsimamishe endapo akifika katika usawa shule ya Msingi Meta ama shule ya Sekondari ya wasichana ya St Francis. Cha ajabu moyo ulikuwa unanidunda sana!

Ilikuwa mithili namfatilia Simba!

Nilifata taratibu huku nikijificha kwenye miti pale nilipoona Evelyne Gando alikuwa anataka kugeuka nyuma. Alipofika pale katika usawa wa shule ya msingi Meta ambako ndipo palikuwa moja ya shabaha yangu kumsimamisha Evelyne Gando. Evelyne alisimama chini ya kivuli cha mti mrefu, nilimshukuru Mungu kwa kuitikia dua yangu nami nikijibanza nyuma ya mti wa mwarobaini.
Ghafla! Nilimuona yule mshenzi!
Richard Chali, akiwa kavaa jeans ya bluu na t-shirt nyeupe, huku kichwa akiwa amevaa kofia ya kapelo. Richard Chali alifika pale aliposimana Evelyne Gando, huku akiwa anabonyazabonyaza simu yake. Alipomkaribia kabisa Evelyne alimkumbatia kwa nguvu huku akimpiga busu zisizo na idadi katika mashavu yake. Niliyashuhudia yote hayo nikiwa pale nyuma ya Mwarobaini. Nilishikwa na hasira yenye mchanganyiko na wivu. Nilitamani nifumbe macho ili nisishuhudie kinachoendelea lakini sikufumba. Ubongo ulikuwa unataka lakini macho yenyewe yalikuwa hayataki.

Baada ya kuongea kwa muda kama wa dakika tano walishikana mikono na kuifuata njia ileile iliyokuwa inaelekea njiapanda ya Mafiat.

Nilichoka sana.
Sura yangu ilisawajika kwa huzuni pamoja na hasira, nilikuwa nataka kulia lakini nilikuwa najizuia kwa nguvu huku nikijiambia kimoyomoyo kuwa
'Sasa kulia kwa ajili ya mapenzi imetosha'
Sikuwa na jinsi kabisa, Evelyne Gando na Richard Chali walinifanyia vitu vibaya sana nikiwa nashuhudia kwa macho yangu yote mawili. Nilirudi nyumbani siku ile nikiwa na hasira nyingi sana. Hasira ambayo sasa ilianza kugeuka taratibu na kuwa CHUKI!
Chuki kwenda kwa Evelyne Gando na baradhuli la kiume Richard Chali.

Nilifika nyumbani nikiwa hoi, nilipitiliza hadi chumbani kwangu na kujitupia kitandani, nililala kifudifudi, huku kichwa changu kikiwa kimelala juu ya mto, nikapitiwa na usingizi, usingizi ambao nilishangaa kwanini ulikuja haraka vile, kwa jinsi nilivyokuwa najisikia sikutegemea kabisa kama nitalala siku ile.
Cha ajabu nililala sana siku ile, nilala saa tatu asubuhi pindi niliporudi kumfatilia Evelyne Gando na kuamka saa tisa jioni. Bahati nzuri wazazi wangu na mdogo wangu Christina hawakuwepo nyumbani siku ile, walienda kukutana na dalali huko Nzovwe, baba alikuwa anataka kununua kiwanja ili nasi tujenge Mbeya.

Saa tisa jioni. Niliamka na kutoka nje, kutafuta kibanda wanachouza chipsi, maana njaa ilikuwa inaniuma sana. Nilikipata, nilikula chipsi nyama na kushushia na soda ya baridi aina ya sprite. Kisha nilirejea nyumbani. Nikaenda tena kitandani kwangu na kujilaza chali, sasa nikaanza kutafakari tukio lilikonitokea asubuhi kule shule ya Msingi Meta. Niliwaza

"Hivi kwanini nalia bila sababu ya msingi. Nalia wakati ninayemlilia hana habari na mimi. Haniwazi. Hajui kama naumia kiasi hiki. Nalia wakati ninayemlilia sijui kama ananipenda ama hanipendi. Pia hajui kama nampenda. Kwanini najitesa kwa kumpenda msichana mmoja tu, Evelyne Gando ilihali wasichana wako wengi sana hapa duniani. Wasichana wazuri pengine zaidi ya Evelyne Gando. Nasema, hii ni mara ya mwisho kulia kwa sababu ya mapenzi, siyo kwa Evelyne Gando tu, ninaapa sitalia tena kwa sababu ya mwanamke yeyote yule duniani!'

Maneno hayo ya mwisho niliyoyatamka kwa sauti ndogo nikiwa nimelala chali pale kitandani. Yalipata baraka katika moyo wangu. Niliamua kwa moyo wangu wote tokea siku ile kuwa sitolia kwa ajili ya mapenzi. Na ilikuwa hivyo, tokea siku hiyo nilimtoa kabisa Evelyne Gando katika kichwa changu!

Naam nilimsahau kabisa Evelyne Gando moyoni. Na nikasahau pia mambo ya wanawake hapa duniani. Sasa nikawa nakumbuka masomo. Nawaza masomo. Nayapenda masomo. Masomo ndio yakawa Evelyne Gamdo wangu. Nilibadilika kabisa, nikawa najibidiisha katika masomo. Sasa masomo yaliuteka moyo wangu kama alivyokuwa ameuteka Evelyne Gando hapo awali. Furaha yangu moyoni ilirejea kwa kasi kubwa sana. Sasa nikawa na furaha kama zamani, kama zile siku za mwanzo zilivyokuwa shuleni Sangu. Nilisahau kila kitu kuhusu rafiki yangu ambaye kwa sasa aligeuka na kuwa adui kwangu, Richard Chali. Nilisahau kila kitu kuhusu mwanaharam yule wa kike, ambaye mwandishi anamwita Evelyne Gando lakini mimi naweza kumwita shetani wa kike.

Ulipita mwezi nikiwa nimesahau hadithi ile mbaya iliyoanza ndani ya basi. Sasa nikawa 'bize' na masomo. Furaha yangu ilirejea kwa kasi kubwa sana. Tofauti kabisa na nilivyofikiria, na afya yangu ilitengamaa, nikaanza kunenepa tena.

*****

Nakumbuka siku moja ya jumatatu jioni nilienda kujisomea katika maktaba ya mkoa Mbeya iliyokuwa kule mjini, Uhindini. Sasa nilikuwa napenda kusoma kuliko kitu chochote kile katika maisha yangu na

nilikuwa naenda maktaba kila mwisho wa wiki kwa ajili ya kujisomea.

Niliingia maktaba, baada ya kumaliza taratibu zote za pale mapokezi ikiwa na pamoja kuonesha kitambulisho changu kilichokuwa kinaniruhusu kuitumia ile maktaba, niliingia ndani ya maktaba. Nikatafuta shelvu ya vitabu vya historia iliyokuwa upande wa kushoto wa maktaba ile na kuanza kutafuta kitabu nilichokuwa nakihitaji. Baada ya muda mfupi nilikiona kitabu nilichokuwa nakitafuta. Kilikuwa kinaitwa" How Europe underdelop Africa' kitabu kizuri kilichoandikwa na mwandishi mahiri Walter Rodney. Nikakiona, nikatafuta sehemu nzuri ya kukaa ili nikisome kitabu hiko kizuri cha historia, nilipata sehemu sahihi nikatulia kwenye kiti na kuanza kukisoma.

Baada ya kama dakika saba ya kusoma kitabu kile, bila kutarajia Ilitokea tu nikacha kusoma kitabu na kuanza kuangalia watu ambao walikuwa wanaingia kwa muda mle maktaba. Niliwaona vijana wawili wakiingia kwa muda ule, mmoja kati ya vijana hao wawili nilimtambua vizuri sana, alikuwa ni Richard Chali! Hasimu wangu mkubwa sana hapa ulimwenguni! Adui yangu wa kweli. Shetani wa kiume. Msaliti mkubwa. Binadamu asiye na urafiki wa kweli. Kiumbe mwenye tabia za mbwa koko...

Nilimuona.

Richard Chali aliingia maktaba na kuelekea upande uleule ambao nilikuwa nimekaa mimi nikijisomea. Wakati yule mwenzie akienda katika upande mwengine kabisa. Richard Chali akitembea kwa mwendo wa kibabe alikuja kukaa siti ya pili toka pale nilipokuwa nimekaa. Bila shaka alikuwa ashaniona. Nami nilimuona vizuri sana lakini sikujishughulisha nae kabisa, sikutaka kumsalimia, na wala sikuwa na haja na salamu yake. Nilijiinamia katika ile meza yangu, kwa umakini mkubwa nikiendelea kusoma kitabu cha Walter Rodney, how Europe underdevelop Africa.
Nilijifanya kama sijamuona kabisa Richard Chali.

Baada ya kama dakika tano kupita, tangu Richard Chali aje kukaa karibu yangu, niliiona mkono ukisogea taratibu pale katika meza yangu, mkono ukatua mezani na kuacha kikaratasi kidogo cheupe, na mkono ule kurejea ulikokuwa awali. Mkono ule ulikuwa mkono wa Richard Chali. Nilikiacha kile kikarasi kikiwa kimekaa pale juu ya meza kwa muda, nilikuwa natafakari nikichukue ama la, nikiache palepale au. Baadae niliamua kukichukua kikaratasi kile, ili nijue kimeandikwa nini na baradhuli yule, rafiki msaliti, Richard Chali.

Nilikifunua taratibu kile kikaratasi, kikaratasi toka kwa Richard Chali. Nikayasoma maneno yaliyoandikwa katika kile kikaratasi kimyakimya. Kiliandikwa maneno matatu tu.

' Hujambo Domo zege'.

Maneno hayo niliyasoma taratibu huku nikitetemeka midomo yangu yote miwili. Yaliniumiza sana. Yalinipandisha hasira toka huko zilizokuwa, na kuzileta pale maktaba. Maneno yale yalinikumbusha kila kitu kuhusu ugomvi wetu mimi, Evelyne Gando pamoja na Richard Chali. Kila nilivyokuwa nakumbuka walivyonifanyia wanyama hawa wawili huko nyuma ndipo hasira zangu zilizidi kututumka katika moyo wangu!

Bila kutegemea wala kufikiria mara mbili, nilinyanyuka pale katika kiti changu nilipokuwa nimekaa na kusogelea katika kiti alichokuwa amekaa baradhuli, Richard Chali, nikiwa nimefura kwa hasira na jazba juujuu!

Niligeuka mbogo!

Nilikuwa naongozwa na hasira. Na mbaya zaidi niliamua ile inaitwa liwalo na liwe. Sikuwa na uwoga hata chembe. Sikuwa na hofu! Nilidhamiria kumfanya kitu kibaya sana Richard Chali! Nilisogea pale katika kiti alipokuwa amekaa baradhuli yule wa kiume. Richard alikuwa amejiinamia katika meza yake akiandika, bila shaka akiandika kikaratasi kingine cha

kunikejeri, labda alimaliza kukiandika, lakini hakufanikiwa kunitumia tena ujinga wake!
Nilimkaribia pale alipokuwa na kumkaba kwa nguvu sana kutokea nyuma kwa kutumia mkono wangu wa kulia! Richard alijaribu kufurukuta lakini hakufanikiwa kuitoa kabali ile, kwa kutumia mkono wangu wa kushoto nilikuwa namshindia migumi ya nguvu ya mbavu! Richard alijitahidi sana kuitoa kabali kimyakimya, thubutu yake! Hakufanikiwa hata chembe. Mkono wangu uling'ang'ania shingo yake mithili ya ruba! Baada ya kama dakika moja ya msuguano huo wa kimyakimya, yule baradhuli akajiona atakufa bure.
Ghafla! alipiga kelele kwa nguvu za kuomba msaada. Huku akinitukana matusi ya nguoni. Mimi nilikuwa kimya, nikitekeleza jukumu langu kwa umakini mkubwa sana. Makelele yake pamoja na matusi yaliyokuwa katika mtindo wa mkoromo yakawafikia wahudumu wa maktaba ile, na nusu ya watu waliokuwa maktaba. Walikuja kwa kasi huku nao wakipiga makelele, ilikuwa tafrani ndani ya maktaba.

Walifika pale tulipokuwa tumeshikana na Richard Chali na kufanikiwa kutuachanisha. Nilikuwa nimevimba sura kwa hasira karibu ya kupasuka! Wahudumu wa maktaba wakatupeleka katika chumba chao. Bila kutusikiliza utetezi wetu walituambia wanatupeleka kituo cha Polisi. Niliogopa sana. Sikuwa

nimewahi kupelekwa polisi kwa kosa lolote lile. Richard Chali nae alikuwa mwoga wa Polisi pia. Baada ya kuomba sana radhi uongozi wa maktaba walitupa zuio la kuingia maktaba ile ya mkoa wa Mbeya katika maisha yetu yote. Huku wakitupa vitisho vya kutupeleka Polisi endapo tusipotii agizo hilo.

Niliondoka ndani ya maktaba nikiwa na hasira kubwa sana. Sasa nilimchukia Richard Chali kuliko hata nilivyokuwa namchukia shetani. Inawezekana kweli nilikuwa na domo zege lakini sikuwa napenda hata kidogo kuitwa jina hilo. Hata Richard Chali alijua chuki zangu juu ya jina hilo.

Nilifika nyumbani nikiwa na hasira vilevile nikisahau hata kuwasalimia wazazi wangu niliowakuta wamekaa pale sebuleni. Nilifika ndani na kujibwaga kitandani kwangu. Nillianza kulia huku nikiwa nimebanwa na kwikwi. Kwa mara nyingine tena Richard Chali alikuwa ananiliza, kwa mara nyingine tena mapenzi yalikuwa yananiliza! Yananitoa machozi! Baada ya muda mfupi wa kulala pale kitandani, nilihisi napapaswa mgongoni, ishara kuwa kulikuwa na mtu chumbani kwangu ananiamsha, niligeuka nyuma taratibu huku sura yangu ikiwa imetapakaa machozi. Nilikuwa natazamana na mama yangu mzazi!

"Vipi mwanangu mbona unalia" Mama aliniuliza kwa sauti yake ya upole.

"Najisikia homa mama" Nilidanganya tena huku nikiangalia darini.

"Homa nd'o inakufanya usisalimie hata wazazi wako?" Aliniuliza tena mama.

"Samahani mama nilipitiwa tu, kichwa kinaniuma sana" Nilidanganya tena.

"Umekunywa dawa sasa" Aliniuliza.

"Nimemeza panadol" "Sawa pumzika, usilie ukilia homa inazidi, umenielewa?"

"Sawa mama"

Mama aliondoka na kuniacha chumbani peke yangu. Nililala pale kitandani bila kupata hata lepe la usingizi. Usingizi utakuja vipi katika hali kama niliyokuwa nayo mimi? Baada ya kuhangaika kitandani kwa muda mfupi, niliinuka na kukaa kitako katika ncha ya kitanda changu. Sasa nami niliamua kupanga mashambulizi yangu kwenda kwa Richard Chali na Evelyne Gando. Niliwaza na kuwazua niwafanye nini watu wale, lakini sikupata jibu la kuuridhisha moyo

wangu. Mwishowe nikaamua niache kuwaza kuhusu wao, na kulala usingizi.

Siku iliyofuata nilienda shule kama kawaida. Niliwakuta wanafunzi shuleni wamechangamka sana, tofauti kabisa na kawaida, wanafunzi walikuwa na furaha isiyo na kifani. Niliulizia sababu ya furaha yao, nilipata jibu, wanafunzi wenzangu walinambia.

'Wanafunzi wa shule ya Sangu watakuja wiki ijayo. Kutakuwa na mashindano ya mpira wa miguu na mpira wa pete, kati yetu na wanafunzi wa Sangu, tangazo liko katika mbao ya matangazo'
Nilihemewa sana!

Taarifa hiyo kwangu ilimaanisha kwamba rafiki baradhuli, Richard Chali na mwanamke msaliti, Evelyne Gando walikuwa njiani kuja shuleni kwetu!
Wanafunzi wote wa shule ya Sekondari Meta walikuwa wanafurahia ujio wa wanafunzi wa shule ya Sekondari Sangu. Kwa maana, Shule ya Sekondari Meta na Shule ya Sekondari Sangu zilikuwa ni shule pinzani sana kuanzia kitaaluma hadi katika michezo. Lakini kwa upande wangu sikujua kama natakiwa kushangilia ama natakiwa kuchukia. Shule ya Sekondari Sangu ndio shule ambayo alikuwa anasoma Evelyne Gando. Shule ya Sekondari Sangu ndio shule ambayo alikuwa anasoma Richard Chali. Shule ya sekondari Sangu ndio

shule ambayo mkuu wake wa shule alikuwa mwalimu Bukuku. Mkuu wa shule ninayemchukia zaidi hapa duniani. Ama hakika sikujua kabisa kama natakiwa nifurahia ujio wa shule ya Sekondari Sangu pale shuleni kwetu? Shule hasimu katika maisha yangu.

Nililala pale kitandani bila kupata hata lepe la usingizi. Usingizi utakuja vipi katika hali kama niliyokuwa nayo mimi? Baada ya kuhangaika kitandani kwa muda mfupi, niliinuka na kukaa kitako katika ncha ya kitanda changu. Sasa nami niliamua kupanga mashambulizi yangu kwenda kwa Richard Chali na Evelyne Gando. Niliwaza na kuwazua niwafanye nini watu wale, lakini sikupata jibu la kuuridhisha moyo wangu. Mwishowe nikaamua niache kuwaza kuhusu wao, na kulala usingizi.
*****

Hatimaye siku ya siku ikafika. Siku ambayo wanafunzi wa shule ya Sekondari Sangu walikuwa wanakuja kwa ajili ya michezo katika shule yetu, shule ya Sekondari Meta.
Pamoja na wanafunzi wenzangu wengi kuwa na furaha isiyo na kifani siku hiyo kutokana na ujio wa shule hiyo lakini mimi sikuwa na furaha hata chembe. Nilitamani nisiende uwanjani kabisa, lakini nilipiga moyo konde, niliamua kwenda uwanjani, na kweli.. nilienda. Nia na

madhumuni ya kwenda uwanjani siku ile sio kwenda kuangalia mpira kati ya shule hizo mbili.
Nia yangu ilikuwa ni kwenda kuangalia ujio wa 'marafiki zangu' wawili, Richard Chali na Evelyne Gando.

Wakati mpira wa miguu siku hiyo ulikuwa unaanza saa kumi kamili ya jioni, mimi saa nane mchana nilikuwa nimeshawasili uwanjani. Nilikaa katika upande wa kaskazini mwa uwanja. Upande ambao watu wengi walikuwa hawapendi kukaa, kwakuwa kulikuwa na nyasi nyingi. Nilijilaza kwenye nyasi nyingi nikiwa sina raha kabisa. Nilitegemea kuja kupigwa pigo kubwa sana na wanaharamu wale, lakini sikuogopa sana, nilijiandaa vyema.

Nakumbuka saa nane na nusu mchana nilisikia muungurumo wa gari. Nikanyanyuka pale nyasini nilipokuwa nimelala na kukaa kitako. Uwanja wa shule ya Sekondari Meta haukuwa na uzio, hivyo ulikuwa unaruhusu gari aina yoyote kuweza kuingia hadi uwanjani. Nililitazama kwa makini sana gari lile, nililitambua!

Lilikuwa gari la la baba yake mzazi, rafiki yangu aliyenisaliti Richard Chali. Nilikuwa nimeshawahi kuliona gari lile mara nyingi sana nilizoenda kumtembelea Richard Chali nyumbani kwao. Nilikaa

vizuri, huku umakini wangu ukiongezeka maradufu. Lengo ni kutaka kujua, ni nani atakayeshuka katika gari lile. Haikuwa mbali sana pale nilipokuwa nimekaa na lilipokuwa limesimama gari lile. Niliweza kushuhudia kila kitu kwa umbali niliokuwepo.
Ndio maana, nilishuhudia kiatu cheusi cha kiume aina ya mkuki moyoni kikitangulia kukanyaga ardhi ya uwanja. Nilinyanyua sura yangu kutoka katika kiatu na kumwangalia mmiliki wa kiatu kile, nilimtambua vizuri sana. Alikuwa ni Mzee Chali. Baba mzazi wa hasimu wangu, Richard Chali !

Baadae kidogo mlango wa kushoto wa mbele wa gari lile ulifunguliwa. Safari hii kilitangulia kiatu cha kike chekundu kugusa ardhi. Naam, kilikuwa chekundu, mchuchumio. Viatu hivyo vilimilikiwa na msichana aliyekuwa amevaa gauni jekundu. Alishuka kwa madaha ya kike huku akitembea kama anaogopa kuikanyaga ardhi. Alilizunguka lile gari la Mzee Chali, na kumfikia Mzee Chali bila ajizi wala uwoga wowote ule. Mzee Chali nae hakuzabaa, alimdaka kwa umahiri mkubwa sana binti yule, binti aliyekuwa na umri sawa na mwanae ambaye kwa sasa alikuwa hasimu wangu, Richard Chali. Walikumbatiana kwa muda mfupi, wakaachiana. Wakapigana mabusu tele kila mahali walipojisikia. Mabusu mashavuni. Mabusu usoni. Mabusu mdomoni. Ilikuwa ni mabusu mabusu mabusu huku mikono ya Mzee Chali ikiwa imekishika vizuri

kiuno cha binti yule. Na yule binti akiwa ameshika mabega ya Mzee Chali. Ilikuwa picha nzuri sana kuitazama. Maana waigizaji walimaliza ufundi wao wakijua wako peke yao. Hakuna jicho lililokuwa linawaona. Kwa bahati nzuri nilipokuwa nimekaa mimi ilikuwa ngumu sana kwa wao kuniona.

Baadae kidogo yule binti aliyevaa gauni jekundu aliingia tena ndani ya gari. Huku Mzee Chali akiwa ameegemea boneti ya gari yake akichezea simu yake ya mkononi. Ilichukua takribani dakika tano yule msichana alitoka tena, sasa hakuwa amevaa lile gauni jekundu. Alikuwa amevaa blauzi jeupe lenye mtindo wa kipekee kiunoni, pamoja na sketi nyeusi. Kitu pekee kilichonifanya nimtambue yule binti kuwa ndiye yuleyule aliyeingia ndani ya gari na gauni jekundu muda mfupi uliopita ni vile viatu vyekundu ambavyo bado vilikuwa miguuni mwake. Nilimwangalia kwa makini sana, usoni, na sasa nilimtambua. Alikuwa ni Evelyne Gando akiwa amevalia sare zake safi za shule ya Sekondari Sangu. Niliziba midomo yangu kwa mikono yangu yote miwili, kutokea pale nilipokuwa. Nikiwa siamini kabisa macho yangu!
Ndio, niliamini macho yangu yananiongopea. Nilimuona Evelyne Gando nae akienda pale mbele ya boneti ya gari, mahali alipokuwa kasimama Mzee Chali, baba mzazi wa hasimu wangu Richard Chali. Alimbusu pajini yule baba ambaye nilikuwa

namuheshimu sana katika maisha yangu huku mikono ya Evelyne Gando ikiwa imekishika vizuri kiuno cha Mzee Chali, wakati mikono ya Mzee Chali nayo ikiwa imekishika vizuri mno kiuno laini cha Evelyne Gando. Nilijisikia hasira sana, safari hii hasira zangu zilikuwa tofauti na nikizozipata mwanzo wa sakata hili, hasira za safari hii zikiwa hazina hata chembe ya wivu. Zilikuwa hasira halisi. Hasira kwa vitendo walivyokuwa wanavifanya Evelyne Gando na Mzee Chali. Niliwaza kimoyomoyo "Inamaana Evelyne Gando anawachanganya mtu na baba yake? kwanini lakini mwanamke huyu amekuwa mnyama namna hii. Hivi ni kweli Richard Chali anajua uchafu huu unaofanywa na Evelyne Gando, msichana anayemwita mpenzi wake? Hivi anajua kweli, kama baba yake mzazi anatembea na mpenzi wake?" Nilijiuliza maswali ambayo sikuwa kabisa na majibu yake.

Nilijiinamia chini kwa huzuni huku nikimuonea huruma sana Richard Chali. Nikimuonea huruma pia mama yake Richard Chali. Sikuweza kabisa kuvumilia chozi la huruma lilinidondoka na kupotelea nyasini.

Niliponyanyua tena sura yangu na kuwaangalia tena wanaharam wale, niliwashuhudia wakiagana na Mzee Chali kuingia katika gari lake na kuondoka, na kumuacha mwanamke yule shetani akiwa kasimama katikati ya uwanja.

Baada ya kama dakika kumi, Richard Chali aliwasili pale uwanjani. Evelyne Gando na Richard Chali walionana wote kwa pamoja. Walikimbiliana kwa furaha kubwa sana na kukumbatiana kwa nguvu.

Nilimuona Richard Chali akisogeza mdomo wake usoni kwa mwanamke yule msaliti kuwahi kutokea hapa duniani na kumpiga busu mahali palepale nilipomshuhudia akipabusu baba yake mzazi muda mfupi uliopita.

Pale nyuma ya goli nilipokuwa nilikuwa natetemeka kwa hasira, sasa nikiwa nimekinaishwa na uchafu uliokuwa unafanywa na msichana huyu, Evelyne Gando. Lakini niliamua kusubiri palepale. Sikutaka kabisa kupelekeshwa na hasira. Nilitulia tuli. Kwa muda ule nilikuwa naangalia picha mbaya sana katika maisha yangu. Na mbaya zaidi nilikuwa shahidi pekee katika jambo zito sana kama lile.
Ndio! Nilikuwa shahidi pekee wa kushuhudia uchafu ule. Baba na mwana wakiwa katika mahusiano ya kimapenzi na mwanamke mmoja. Kwa bahati mbaya zaidi nilikuwa shahidi lakini adui!
Shahidi adui!

Nilikuwa sipatani na Evelyne Gando, nilikuwa sielewani na Richard Chali. Wote walikuwa maadui

wakubwa kwangu. Ni nani angeukubali ushuhuda wangu? Kwanza ningemwambia nani habari ile mbaya kabisa. Ama hakika ulikuwa mtihani mkubwa sana kwangu. Kuwa na siri nzito inayowahusu maadui zangu.

Baada ya lile busu kutoka katika mdomo wa Richard Chali kwenda katika shavu laini la Evelyne Gando waliachiana. Kisha wakatazamana kwa muda mfupi. Pale nilipokuwa niliona midomo yao ikichezacheza, bila shaka walikuwa wakijadiliana jambo. Umbali niliokuwepo haukuruhusu kusikia kitu walichokuwa wanaongea. Baada ya maongezi hayo ambayo nilikuwa sijasikii yaliyochukua kama dakika tatu walikumbatiana tena.
Wakabusiana tena.

Nikiwa pale nilipokuwa nilitamani nitoke pale nyasini niende mahali pale. Ili kumueleza uchafu uliokuwa unafanywa na mwanamke yule mbaya kabisa, Evelyne Gando mahali palepale, lakini nani angenielewa. Mimi na Richard Chali sasa tulikuwa maadui wakubwa sana, asingeweza kunielewa kabisa!

Baada ya muda mfupi wa kuongea walitoka pale katikati ya uwanja na kwenda pembeni mwa uwanja.
Walikaa chini.

Wakiendelea na maongezi yao. Kutoka pale nilipokuwa nimekaa nilisikia mlio wa gari, gari la wanafunzi wa shule ya Sekondari Sangu likiingia pale uwanjani. Waliingia kwa shangwe na kelele nyingi sana, huku wakisindikizwa na nyimbo, nyimbo ambazo nazo zilikuwa katika mfumo wa kelele. Muda huohuo wanafunzi wa shule ya Sekondari Meta nao walikuwa wanakuja uwanjani makundi kwa makundi huku wakiwazomea wanafunzi wa shule ya Sekondari Sangu. Waliokuwa wanaingia na gari yao.
Ilikuwa tafrani.

Nilitumia kama dakika tatu kuyashuhudia na kuyasikia yote hayo. Dakika ya nne niligeuka pale walipokuwa wamekaa Evelyne Gando na Richard Chali.
Evelyne Gando hakuwepo!
Evelyne Gando alikuwa kayeyuka mithili ya upepo. Niliangaza macho yangu huku na huko kumtafuta Evelyne Gando. Lakini sikumuona kabisa. Nikaachana nae, akili yangu iliacha kumtafuta mwanamke yule msaliti, Evelyne Gando. Macho yangu sasa yalibadili uelekeo, sasa yakaelekea katika gari kubwa aina ya fuso, gari ambayo ilikuwa wanashuka wanafunzi wa shule ya sekondari Sangu. Walishuka, wakashuka. Mwanafunzi wa saba kushuka katika gari ile, macho yangu yalivutika nae, yakawa yameganda kwake, yakifata nyendo zake. Nilimuona mwanafunzi yule

akitua chini salama. Akiwa na begi dogo mkononi. Akasimama kidogo, akageuza shingo yake upande wa kulia, akaangalia upande huo kama nusu dakika, akageuza shingo yake kuangalia upande wa kushoto, nako aliangalia kama nusu dakika. Akapiga hatua moja ndogo kwa mguu wake wa kulia, mguu wa kushoto nao ukafata kupiga hatua ukipishana na ule mguu wa kulia. Alikuwa anafanya kitu kinachoitwa mwendo. Kutembea. Baada kama ya hatua sita mwanafunzi yule alisimama. Aligeuka upande wa kushoto haraka. Alitabasamu. Alitanua mikono yake huku akiwa na tabasamu tele usoni mwake. Mara, nilimuona msichana akikirukia kifua cha kijana yule, na kupata kumbato la nguvu. Macho yangu yalihama ghafla toka kwa watu wale waliokumbatiana, na kutua katika ile gari ya fuso ambayo bado wanafunzi walikuwa wanaendelea kushuka. Sasa Ilikuwa zamu ya mwanafunzi wa kiume kushuka katika gari ile. Kwa bahati mbaya kabisa kijana yule alikuwa akishuka huku akiangalia wale vijana waliokumbatiana katikati ya uwanja. Kijana alipoteza kabisa umakini. Alikuwa analishangaa kumbato. Bila kutegemea yule kijana aliporomoka toka kule juu ya gari hadi chini. Unajua lile kumbato lilikuwa la kina nani? Lilikuwa kumbato la mwanamke msaliti, anayesaliti mtu na baba yake kwa pamoja. Mwanamke anayeishi kwa wakati mmoja na mtu na mwanae. Sasa Evelyne Gando alikuwa kifuani kwa mwanaume aitwae Philimon Uvambe,

mchezaji bora wa mpira kwa shule ya Sekondari Sangu. Lilikuwa ni kumbato la mwanamke msaliti ndilo lililomdondosha kijana yule toka garini. Evelyne Gando alikuwa kamuacha Richard Chali pale chini, na sasa yupo na mwanaume mwengine.

Yule mwanafunzi aliyeanguka aliinuka huku akichekwa na wanafunzi wenzie. Macho yangu yalitoka kule kwenye gari na kurudi katika kumbato la mwanamke msaliti, Evelyne Gando. Sasa alikuwa anaachiana na yule mwanaume, Philimon Uvambe.

Mkono wa kushoto wa Evelyne Gando na mkono wa kulia wa Philimon Uvambe ilishikana kwa nguvu na miili iliyokuwa inamiliki mikono ile ilijongea na kuelekea pembeni ya uwanja. Upande tofauti na ule aliokuwa amekaa Richard Chali. Walichagua sehemu waliyoiona wao sahihi na kukaa chini. Nami nilisimama toka pale nililokuwa nimekaa, na kwenda kujichanganya na wanafunzi wenzangu.

Majira ya saa kumi na nusu mpira ulianza. Ilikuwa ni mechi ngumu sana. Iliyokutanisha shule mbele mahasimu jijini Mbeya. Shule ya Sekondari Sangu na shule ya Sekondari Meta. Shule hizi mbili zilikuwa mahasimu kweli, mahasimu katika michezo, mahasimu katika taaluma. Hadi mpira unamalizika mpira ilikuwa sare ya moja kwa moja. Kutokana na mwingiliano wa

watu baada ya mpira kumalizika sikuwaona wale maadui zangu wawili. Siku hiyo niliyogundua mambo mabaya sana kuhusu Evelyne Gando ilipita. Tangu siku hiyo sikukutana tena Evelyne Gando wala Richard Chali. Ni miezi takribani sita ilipita tangu mambo hayo yatokee.

*****

Mimi ni mpenzi mkubwa sana wa kuangalia mpira. Napenda sana kuangalia mpira wa miguu. Siku moja ya mwisho wa wiki ilimikuta katika uwanja wa Sokoine. Uwanja mkubwa na maarufu zaidi katika Jiji la Mbeya. Nakumbuka kulikuwa na mechi kati ya timu ya Magereza ya Prisons, timu yenye maskani yake katika gereza la Luanda walikuwa wanacheza na timu ya Yanga, timu yenye maskani jijini Dar es salaam. Niliwahi kufika uwanjani ili nipate mahali pazuri pakukaa. Maana mara nyingi inapokuja kucheza Simba au Yanga uwanja wa Sokoine hufurika sana. Nilikaa upande unaoangalia geti kuu la kuingilia uwanjani. Upande ambao unatazamana na mahali wanapokaa viongozi ama watu mashuhuri. Ndipo niliwaona! Evelyne Gando akiwa na Mzee Chali walikuwa katika jukwaa hilo la VIP. Toka pale nilipokuwa niliziona vizuri sana tabasamu zao za furaha. Kwa mara nyingine tena nilithibitisha kwamba wale watu walikuwa ni zaidi ya mtu na mkwewe.

Nilithibitisha kwamba Mzee Chali na Evelyne Gando walikuwa mtu na mpenzi wake. Sikutaka kabisa kuimezea ile habari ya kusikitisha. Habari ya aibu. Shida sasa ilikuwa nitaiambia vipi jamii ili inielewe. Je jamii haitohusisha ugomvi wangu na Richard ndio sababu iliyofanya nitunge mambo hayo. Nilitatizika sana.

Ilikuwa asubuhi na mapema. Wiki moja baada ya tukio la kule katika uwanja wa wa mpira wa Sokoine. Nakumbuka ilikuwa siku ya jumamosi, na nilipanga siku hiyo iwe siku ya kufichua ukweli. Kumwaga mchele hadharani. Kumuonesha Richard Chali kwamba Evelyne Gando ni nani. Niliamua ile inaitwa liwalo na liwe!

Siku hiyo nilitoka asubuhi na mapema sana na kuelekea nyumbani kwa kina Richard. Nilipanga kwenda kumwambia kila kitu mama mzazi wa Richard, mke wa mzee Chali. Nusu saa baadae nilikuwa nje ya geti la kina Richard, niligonga mlango na kusubiri kufunguliwa. Nilisikia kelele za miguu ya mtu zikija kufungua mlango. Na geti lilifunguliwa taratibu. Nilimuona mtu aliyekuja kufungua mlango.
Adui yangu!

Tulikuwa tunatazamana uso kwa uso na Richard Chali. Rafiki yangu wa zamani ambaye sasa ni hasimu wangu mkubwa!

"Nambie we domo zege, umepotea njia?" Richard aliniuliza kwa kejeri na dharau kubwa sana.

Niliposikia hilo jina hasira zilinishika maradufu. Jazba zilinipanda hasaa. Nilikasirika. Sikulipenda hilo jina hata kidogo. Lilikuwa ni jina baya zaidi kusikiwa na masikio yangu. Nilianza kumwangalia kwa jicho la chuki!

Ghafla nikamshika Richard shingoni na kumsukumia ndani kwa nguvu. Kilikuwa ni kitendo cha ghafla sana ambacho Richard hakukitegemea kabisa. Alijikuta akidondoka chini huku mimi nikiwa nimesimama mbele yake.

"Nyi watoto vipi tena!" Nilisikia sauti ya mama Richard Chali ikiuliza toka bustani, iliyokuwepo ndani ya uwa.

"Nina shida na wewe mama.." Nilisema huku nikielekea upande wa bustani. Nikimuacha Richard pale chini. Akiwa pale chini Richard aliniangalia kwa jicho lenye hasira sana. Nilisikia akinitukana tusi

kubwa la nguoni kwa sauti ndogo, nilisikia lakini mama yake hakusikia. Lakini mimi wala sikujari.

"Hivi mna nini hivi nyi watoto?" Kwa sauti ya kulalamika mama Chali aliuliza tena.

"Evelyne, Evelyne Gando mama!" Nililitaja jina la Evelyne kwa nguvu. Jina ambalo lilimtoa mbio baba yake Richard huko alikokuwa na kutoka nje. Sasa tulikuwa watu wanne nje ya nyumba ya kina Richard, uwani. Richard alijitahidi kujizoazoa pale chini na kutufuata kule upande kulikokuwa na bustani, na mzee chali na alikuja upande huohuo. Mzee Chali akiwa anahema vibaya mno, Richard akiwa anahema vibaya sana, mama Chali akiwa na mshangao mkuu usoni mwake. Hakuwa anaelewa kabisa jinsi mambo yalivyokuwa yanaendelea pale uwani.

Ghafla katika mlango wa geti alisimama mtu mwengine wa tano, alikuwa ni mtoto wa kike aliyeumbwa ukaumbika. Alikuwa ndani ya suruali ya njano ya jeans na blauzi fupi nyeusi. Alikuwa amesimama huku mkono mmoja akiwa kalishikia geti. Kwa majina mwanamke aliyesimama getini alikuwa anaitwa Evelyne Gando!

'Evelyne!" Richard na baba yake waliita kwa pamoja. Kilikuwa ni kindumbwendumbwe!

Pale mlangoni Evelyne Gando alipigwa na butwaa. Alikuwa anatazamana na wapenzi wake wawili kwa mpigo. Alisimama wima huku mkono wake wa kulia ukiwa unaliachia geti sasa.

"Evelyne Gando" Niliita hilo jina huku nikielekea pale mlangoni alipokuwa.

Macho sita toka kwa watu watatu yalikuwa yanauangalia mgongo wangu. Macho ya mzee Chali, Mama Chali na Richard.

"Nimepatikana leo!" Evelyne alitamka kwa nguvu.

Alikuwa anadondoka chini. Nilikimbia kwa kasi na kumuwahi kabla hajafika sakafuni. Mikono yangu ilimshika mwanamke yule mrembo niliyekuwa nampenda sana hapo kabla. Nilijisikia wa thamani sana, ilikuwa kama nimeshika dhahabu. Evelyne aliniangalia kwa jicho lilionesha kukata tamaa.

"Naombea unisaidie" Nilimsikia akitamka kwa sauti ndogo sana. Richard na wazazi wake walikuja mbio pale mlangoni. Wote wakiwa wamechoka na mambo yale.

"Na mimba yako mzee" Evelyne alithubutu kusema huku akilia, alisema huku macho yake yakimwangalia mzee Chali.

"Unasemaje Eve, una mimba ya baba?" Richard aliuliza huku machozi yakimtoka. Nakwambia alilia. Kauli ile ya Evelyne haikuweza kuvumiliwa na mama Chali, alianguka chini vibaya sana, yeye hakukuwa na wa kumdaka. Mzee Chali alivyoona vile alichanganyikiwa sana. Lakini hakuwa na la kufanya, chozi la majuto lilimdondoka.

"Richard kaite Tax?" Nilisema kwa nguvu. Richard alikuwa ananiangalia tu huku akitetemeka, hakuwa na la kufanya. Machozi yalikuwa yanatiririka toka machoni mwake.

Niliona hatari iliyokuwa inatukaribia mahali pale. Taratibu nilimuweka Evelyne chini na kukimbilia nje ya geti. Dakika kama kumi na tano baadae nilirejea pale, nyumbani kwa mzee Chali.
Niliyoyakuta!
Lile eneo lote lilikuwa limetapakaa damu. Damu tupu! Mzee Chali alikuwa amelaliana na mkewe, wamekumbatiana, wote wakiwa wametapakaa damu vibaya mno. Evelyne Gando hakuwepo pale. Nilijaribu kumtafuta kwa macho lakini sikumuona. Huku

Richard Chali akiwa amelala pembeni kabisa ya bustani akigugumia kwa maumivu.
Eneo lilikuwa na damu, damu ambayo bila shaka ilisababishwa na mapenzi. Mapenzi yalifarakanisha ile familia, familia yenye kila sababu ya kuitwa familia bora. Mapenzi, mapenzi mabaya sana. Mapenzi yana nguvu sana. Nguvu ya mapenzi haina kifani. Baba na mwana waliokuwa wanapendana sana bila shaka walipigana kwa sababu ya mapenzi. Sijui kilikuwa kimetokea nini na kwa muda gani. Lakini mwili wa mzee Chali ulikuwa umetapaa majeraha ya kisu. Mwili wa Richard Chali nao ulikuwa una majeraha makubwa ya kisu. Cha ajabu Evelyne Gando haukuwepo eneo lile.
Sikumuona.

Baada ya nusu saa askari Polisi waliwasili pale nyumbani. Sikujua nani aliyewaita. Baada ya kupekua ndani na nje ya nyumba walifanikiwa kuukuta mwili wa Evelyne Gando ukiwa bustanini, ukiwa na majeraha mengi sana, ukiwa hauna uhai. Wale majeruhi wawili walipakiwa katika gari la Polisi na kupelekwa hospitalini, lakini hawakufika, walifia njiani. Baba na mwana walikufa kwa sababu ya mapenzi.

Saa tano mbele mama Chali alizinduka. Kumbe hakuwa ameumia hata kidogo. Damu alizokuwa nazo

zilitoka kwa Mzee Chali. Nilimsimulia kila kitu kilichotokea hadi kutokea kwa mambo yale. Alilia sana. Alisikitika sana. Lakini hakuwa na jinsi, mambo yalikuwa yashatokea. Baada ya siku tatu maiti ya Richard Chali na baba yake zilisafirishwa kwao. Na Evelyne Gando alizikwa katika makaburi yaliyopo nyuma ya Shule ya Sekondari Mbeya. Nililia sana wakati tunamzika Evelyne Gando. Nilikumbuka ile siku ya kwanza tunaonana ndani ya basi. Nilikumbuka ile siku ya 'debate'. Siku ya kwanza kumkumbatia Evelyne. Mwanamke aliyezitesa sana hisia zangu. Tulimzika Evelyne. Nikikuwa mfu wa mwisho kutoka katika tuta la kaburi lake. Nikipiga magoti. Nilinyoosha mikono juu nikimuombea kwa Mungu apumzike kwa amani Evelyne. Mara askari walinivamia na kuninyanyua pale. Baada ya utambulisho, nilitambua kwamba natakiwa niende Polisi nikaelezee juu ya mambo yale. Ndani nyuma ya gari ya Polisi nililia kwa nguvu huku nikisema kwa sauti kubwa. Kwa mkasa huu kamwe SITOISAHAU MBEYA!

*****

Jitihada za baba. Ushahidi wangu na wa mama Chali na maombi yangu kwa Mwenyezi Mungu ulifanya niachiwe huru baada ya kukaa mahabusu kwa muda wa mwezi mmoja. MWISHO